**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA HANDENI MJI**

Tarehe 16, Februari 2023

# TANGAZO LA KAZI YA UJENZI WA JENGO LA DHARURA (EMD) HOSPITALI YA WILAYA YA HANDENI

**LGA/172/2022/2023/FA/W/02**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Handeni anatangaza Nafasi ya Kazi ya ujenzi wa jengo la Huduma ya Dharura (EMD) katika Hospitali ya Wilaya ya Handeni.

Halmashauri ya Handeni Mji inapenda kualika **Kampuni, Ushirika, Taasisi za Serikali au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria,** wenye nia na uwezo wa kujenga jengo la Dharura (EMD) katika Hospitali ya Wilaya ya Handeni kutuma maombi ya kazi hiyo bila kusita.

**SIFA ZA MWOMBAJI:**

1. MWOMBAJI AWE NA CHETI CHA UJENZI DARAJA LA SITA (Class six) AU ZAIDI
2. MWOMBAJI AWE NA UZOEFU WA UJENZI WA MAJENGO MAKUBWA YA SERIKALI *{AONESHE VIAMBATA - BARUA/MKATABA ALIOPEWA NA MWAJIRI WA KAZI YA UJENZI KWENYE TAASISI YA SERIKALI}*
3. MWOMBAJI AWE NA UWEZO WA KUSOMA MICHORO YA JENGO, KUIELEWA NA KUITAFSIRI

4. MWOMBAJI AWE NA UWEZO WA KUAJIRI **MAFUNDI WASIOPUNGUA KUMI {10} AWE NA UWEZO WA KUWALIPA BILA USUMBUFU**

5. MWOMBAJI AWE NA **MAFUNDI** WENYE UWEZO WA KUTAFSIRI RAMANI NA KUITEKELEZA

6. AWE HAJAWAHI KUSHINDWA KUFANYA KAZI ALIZOPEWA NA KUWA ANAO UWEZO WA KUMALIZA KAZI KWA WAKATI

7. ASIWE NA MADENI YANAYOWEZA KUHARIBU UTENDAJI WA KAZI KATIKA TAASISI ZA UMMA

BARUA YA MAOMBI **YENYE NAMBA YA SIMU YA MWOMBAJI** IWEKWE NDANI YA BAHASHA ILIYOFUNGWA KWA LAKIRI. JUU YA BAHASHA IONESHE KAZI INAYOOMBWA, NAMBA YA ZABUNI NA ZITUMWE KWA MKURUGENZI KWA ANWANI IFUATAYO:

***MKURUGENZI WA HALMASHAURI***
***YA MJI HANDENI***
***S L P 51***
***HANDENI***

**MASHARTI YA KUOMBA**

**Maombi ya Kazi yazingatie masharti yafuatayo:-**

- Barua za maombi na BOQ ya gharama za fundi zitapokelewa katika ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi iliyopo katika jengo la Halmashauri ya Handeni Mji mtaa wa Kilole kuanzia siku ya Alhamisi **tarehe 16 /2/ 2023** na kuwekwe kwenye sanduku la Tenda

- Halmashauri imepanga siku ya jumanne tarehe 22 Februari 2023 saa 4.00 asubuhi iwe siku ya waombaji kuoneshwa eneo la mradi

- BOQ ya kazi na Michoro ya jengo inapatikana katika ofisi ya Manunuzi na Ugavi kwa gharama ya shilingi 100,000.00 itakayolipwa kwa control namba ya Halmashauri. Fedha hiyo haitarudishwa.

- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni siku ya Jumatano tarehe 01/3/2023 saa 4:00 asubuhi. Baada ya hapo hakuna barua yoyote itakayopokelewa

- Kwa maelezo zaidi fika Halmashauri ya Mji Handeni ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi

- Waombaji au wawakilishi wao, wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa nukuu za bei BOQ utakaofanyika tarehe 01 Machi 2023, saa 4.00 asubuhi katika Ukumbi wa Halmashauri ya Mji Handeni

Maryam Ukwaju
**MKURUGENZI**
**HALMASHAURI YA MJI HANDENI**

MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
S. L. P 61
HANDENI